# Uanzishwaji wa vituo vya tiba dhidi ya dawa za kulevya ulivyosaidia kuokoa vijana katika lindi la uteja



*VIJANA wakiwa wanajidunga sindano zenye dawa za kulevya.*

> "Tafiti za kisayansi zinaonesha mraibu (mtumiaji wa dawa za kulevya) anayepata mseto wa huduma ya tiba kwa kutumia dawa na unasihi anakuwa kwenye nafasi ya kupata nafuu mapema zaidi kuliko yule anayetumia dawa bila unasihi au unasihi bila dawa.
>
> **Kamishna wa Kinga na Tiba wa Mamlaka Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Peter Mfisi**

**Na REHEMA MAIGALA**

SERIKALI inaendelea kusimamia na kuboresha utoaji wa tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya katika vitengo vya afya ya akili vilivyo katika hospitali mbalimbali nchini.

Lengo la kufanya hivyo ni kuona rasilimali watu inapungua kwa kujidumbukiza katika utumiaji wa dawa ya kulevya na kusababisha Taifa kupunguza waleta maendeleo.

Uanzishwaji wa vituo hivyo vya tiba, ambavyo vimekuwa mkombozi mkubwa kwa watumiaji na vimepunguza kasi ya watumiaji wa dawa hizo.

Akizungumza katika makala hii, Kamishna wa Kinga na Tiba wa Mamlaka Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Peter Mfisi anasema uraibu wa dawa za kulevya unatibika kwa kutumia dawa za hospitali pamoja na usaidizi wa ushauri nasaha unaojulikana kitaalamu kama Medically Assisted Therapy (MAT).

Anasema mseto huo wa dawa na ushauri nasaha ni huduma iliyothibitishwa kisayansi na inaonekana kuleta tija zaidi katika tiba na kuleta mabadiliko chanya katika upataji nafuu miongoni mwa waraibu.

"Tafiti za kisayansi zinaonesha mraibu (mtumiaji wa dawa za kulevya) anayepata mseto wa huduma ya tiba kwa kutumia dawa na unasihi anakuwa kwenye nafasi ya kupata nafuu mapema zaidi kuliko yule anayetumia dawa bila unasihi au unasihi bila dawa.

Anaongeza dawa zinazotumika kutibu waraibu kwa sasa ni methadone, buprenorphine na naltrexone lakini kwa sasa dawa zinazotumika ni methadone na buprenorphine" anasema Kamishna Mfisi.

Anasema huduma ya tiba ya methadone na ushauri nasaha kwa waraibu wa dawa za kulevya ilianza rasmi mwaka 2011 na Tanzania ilikuwa ya kwanza kutoa huduma hiyo upande wa Bara la Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Vilevile, huduma hiyo huhusisha utoaji wa tiba za magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile ugonjwa wa akili, ukimwi, kifua kikuu, magonjwa ya ngono na homa ya ini.

Aidha, anasema vituo hivyo hutoa huduma zingine kama vile tiba kwa watoto waliozaliwa na tatizo la uraibu kutoka kwa mama zao,uzazi wa mpango na tatizo la udumavu pamoja na magonjwa ya kinywa.

Anasema kwa kipindi cha mwaka 2020, idadi ya waraibu waliopata tiba katika vitengo vya afya ya akili ni 169,269 .

Anasema serikali inaendelea kuongeza nguvu katika eneo hili la tiba ya methadone na kujenga vituo vingine zaidi kulingana na uhitaji na uwezo uliopo.

Anasema hadi mwisho wa mwaka 2020, vituo

> "Lengo la kufanya hivyo ni kuona rasilimali watu inapungua kwa kujidumbukiza katika utumiaji wa dawa ya kulevya na kusababisha Taifa kupunguza waleta maendeleo. Uanzishwaji wa vituo hivyo vya tiba, ambavyo vimekuwa mkombozi mkubwa kwa watumiaji na vimepunguza kasi ya watumiaji wa dawa hizo.




*Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Gelard Kusaya*

vitano vipya vilikuwa katika hatua ya mwisho ya ujenzi kwa ajili ya kuanza kutoa huduma mapema mwaka 2021 katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam .

Kamishna alitaja idadi ya waraibu kuanzia mwaka 2011 hadi 2020 ni 9,188, ambapo wanaume ni 8, 680 na wanawake 508 kati ya hao waraibu waliokutwa na na maambukizi ya VVU 932 kati yao wanaume 732 na wanawake 200 vilevile waraibu waliokutwa na ugonjwa wa kifua kikuu ni 550 wanaume 504 na wanawake 46.

Licha ya kuwepo kwa baadhi ya hospitali za serikali zinazotoa huduma ya tiba kwa waraibu wa madawa ya kulevya lakini kuna vituo binafsi ambavyo navyo hutoa huduma hiyo lengo likiwa ni kupunguza kasi ya watumiaji wa madawa hayo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu aneyeshughulikia Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi anaelezea madhara ya dawa za kulevya kwa vijana jinsi linavyoathiri Taifa.

Anasema utumiaji wa dawa za kulevya yana athari kubwa kwa vijana kwa sababu anafanya vitu ambavyo si lengo lake kuvifanya na yanamsababishia kupoteza ndoto yake aliyojipangia tangu alivyokuwa mtoto mdogo.

Naibu Waziri Katambi anasema mtu yeyote akitumia dawa hizo unakuwa hayupo katika ufahamu wa kawaida hivyo anaweza kushawishika kujiingiza katika ugaidi, wizi na ngono zembe ambayo itamsababishia kupata maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi na magonjwa mengine yanayotokana na zinaa.

" Dawa za kulevya yanaathari kubwa kwa jamii na hata taifa, hivyo wazazi na walezi tunatakiwa tuwe na malezi bora kwa watoto wetu ili wasiweze kujitumbukiza katika kundi hilo"anasema Naibu Waziri Katambi.

Naibu Waziri Katambi anasema serikali inafanya jitihada nyingi kuhakikisha uingiaji wa dawa za kulevya unakuwa ni mgumu ndani ya nchi na wanaendelea kujenga majengo mengi kwa lengo la kuwapa tiba wale wanaotumia dawa hizo

Anasema hata ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), imeeleza madhara makubwa yatokanayo na dawa za kulevya katika nchi hata dunia kwa ujumla.

Naye, Mratibu wa Kituo cha Kutunza Waraibu hao (Sobber House) kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam, Juma Mhina, anasema lengo la kituo chao ni kuiona Tanzania inakuwa na vijana shupavu kwa ajili ya kuleta maendeleo .

Anasema kituo chao kinahudumia kwa kufuata mpangilio wa hatua 12 wa usitiri wa pombe na mihadarati ikiwemo kumpeleka mtumiaji wa dawa za kulevya katika hospitali ya serikali au kituo cha afya kwa ajili ya kupata huduma ya Detoxification.

Anasema huduma hiyo inasaidia kuondoa alosto katika mwili wa mtumiaji na maumivu katika mwili wake kwa sababu mtumiaji hawezi kuacha dawa ghafla tu ila anaacha kwa kufuata hatua zilizopo ikiwemo kupata ushauri nasaha kutoka kituoni hapo.

Mhina anasema kituo chao kinatoa tiba ya muda wa miezi sita hadi mwaka mmoja na katika kipindi hicho wanatoa elimu kuhusu athari za dawa hizo.

Pia, anasema wanatoa huduma za kidini kwa upande wa Kiislamu na Kikristo ili kuwaweka kiimani watumiaji hao

"Licha ya kutoa huduma mbalimbali pia tunatoa huduma ya ujasirimali ili mtumiaji anapomaliza muda wake wa kukaa katika kituo hiki akienda nyumbani aweze kujiajiri mwenyewe kwa kutengeneza sabuni, mishumaa na hata kufuma vitambaa kwa upande wa wanawake"anasema

Anasema ni kweli mtumiaji wa dawa za kulevya hakitoka katika kituo hicho anakuwa hana hamu tena ya kutumia au kunywa pombe kupita kiasi kutokana na elimu aliyoipata.

> **"Mara nyingi tunavyokuwa na waraibu katika kituo tunawasiliana na familia yake kujua alikuwa anaishi vipi kabla hajaanza kutumia dawa ili na sisi tuweze kumkumbusha yale maishayake ya awali kwa ajili ya kurudi katika hali yake ya awali...**
>
> **Mratibu wa kituo cha kutunza waraibu hao**

Anasema hiyo inatokana na elimu inayotolewa na wataalamu wa kituo hicho ambao pia hutoa elimu hata kwa familia zilizoathirika (Family Therapy).

"Mara nyingi tunavyokuwa na waraibu katika kituo tunawasiliana na familia yake kujua alikuwa anaishi vipi kabla hajaanza kutumia dawa ili na sisi tuweze kumkumbusha yale maishayake ya awali kwa ajili ya kurudi katika hali yake ya awali.

Naye, Nestory Benno (37) ni muathirika wa dawa za kulevya toka mwaka 2003 hadi 2014 alipoanza kutumia dawa ya methadone katika Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala.

Anasema ametumia dawa hizo kwa kipindi cha miaka 11 kwa wakati huo alikuwa mwalimu wa shule ya sekondari, akifundisha kidato cha pili na tatu.

Nestory anasema, alikuwa mwalimu mzuri na hakuna mtu yeyote aliyewahi kujua kuwa anatumia dawa hizo.

Anasema ingawa hakuna mtu aliyejua kuwa anatumia dawa za kulevya lakini yeye mwenyewe alikuwa anajisikia vibaya akiwa amekosa madawa hayo hivyo huamua atoroke au kuomba ruhusa yeyote ili akapate dawa.

Ilivyofika mwaka 2014 aliamua kwenda hospitali kwa ajili ya kutumia dawa ya methadone.

"Uamuzi wangu ulikuwa sahihi ingawa nilikosa kazi lakini nilivyoanza kutumia methadone tu nilianza kujiona kuwa na mimi nipo dunia sawa sawa na sio kama ile ya awali"anasema .

Anasema alipoanza kutumia dawa ya methadone mara alianza kusikia njaa na kupata hamu ya kula, mwili wake ulikuwa mwepesi na hakuna maumivu aliyokuwa anayapata katika mwili wake.

"Hapo awali nilikuwa sisikii njaa, sipati usingizi na nilikuwa napenda nikijiona mchafu kuliko niwe msafi"anasema.

Anasema methadone imemsaidia kwa kiasi kikubwa hadi hivi sasa anafanya shughuli zake za kumuingizia kipato.

"Nilivyoanza kutumia dawa ya methadone nililazimika kuacha kazi kwa sababu nilikuwa nahitajika hospitali asubuhi sana hivyo niliamua kuacha kwa sababu sikutaka mtu ajue matatizo yangu"anasema.




*KIJANA Nestory Benno aliyekuwa anatumia dawa za kulevya aliacha baada ya kutumia dawa ya methadone.*